# Prayer

**Chimala Mission**
**Seminar**
**JUNE 1998**

# Sala

**Yaliyomo** **Uka.**


1. Umuhimu Wa Sala - B.J.M. Kulanga 03

2. Jinsi Maombi Yanavyotakiwa Kuwa Na Jinsi Yasivyotakiwa Kuomba - Lazima Newton 04

3. Hali Ya Maombi Yanayokubaliwa #1 - Heath Stapleton 06

4. Hali Ya Maombi Yanayokubaliwa #2 - Heath Stapleton 07

5. Hali Ya Maombi Yanayokubaliwa #3 - Heath Stapleton 08

6. Vizuizi Vya Maombi Yanayokubalika - Linkosi Mkwana 09

7. Vitu Tunavyoweza Na Tungeweza Kuomba (kusali) Kwa Ajili Yake #1 - Ken Brown 12

8. Vitu Tunavyoweza Na Tungeweza Kuomba (kusali) Kwa Ajili Yake #2 - Boaz Kasiba 14

9. Tabia Katika Sala (Maombi) - B.J.M. Kulanga 15

10. Baadhi Ya Matatizo Katika Maombi - Joshua Mwakyasima 18

11. Je, Mungu Anajibu Maombi - Peter Kamatula 22

12. Vipi Kuhusu Maisha Yako Ya Maombi? - Heath Stapleton 26

## Umuhimu Wa Sala

*Utangulizi*:

1. Kanisa la sasa lina matatizo mengi ya aina ile ile kama wanafunzi waliyokuwa nayo bustanini.
    a. Wakati Bwana alikuwa anaomba, wao walikuwa wanasinzia, Mt. 26:36-40.
        1) "Sisi ni kizazi cha watakatifu wasioomba."

2. Maombi (sala) ni muhimu kwa kila mkristo kwa sababu ni sehemu muhimu ya maisha anayotutaka Mungu tuishi.
    a. Kushindwa kuomba ni dhambi, 1 Sam. 12:23.
    b. Angalia maandiko haya, Lk. 18:1; 21:36; Flp. 4:6; Kol. 2:2; 1 Kor. 7:5.

3. Kusudi la somo hili ni kusisitiza umuhimu wa sala.

*Somo lenyewe*:

I. Watu wa Mungu waaminifu kupita wote katika Agano la Kale walikuwa watu wa maombi.
    a. Ibrahimu: Mwa. 15:1-6; Mwa. 18:22-32.
    b. Musa: Kut. 8:12, 13; 32:30-35; 33:13; Hes. 12:12, 13.
    c. Samweli: 1 Sam. 8:1-7; 12:19-23; 15:11.
    d. Daudi: 2 Sam. 7:18-20; 12:16.

II. Yesu aliomba mara nyingi.
    a. Yesu aliomba (alisali): Lk. 3:21; 6:12-13; Mt. 14:23; Yn.17; Mt. 26:36-44; Lk. 23:34.
    b. Kama Yesu, Mwana wa Mungu asiye na dhambi, alitambua haja ya maombi (sala) na thamani yake, sisi tunapaswa tujali kiasi gani?

III. Mitume na kanisa la awali walisali mara nyingi.
    a. Mdo. 2:42; 3:1; 4:23-24; 6:1-4, 6; 8:15; 9:40; 10:9; 12:1-5; 13:1-3; 14:23; 16:25; 20:36.

*Mwisho*:

Kutokana na mifano tunaona umuhimu wa kuomba (kusali).

Asante: Robert Stapleton

**Jinsi Maombi Yanavyotakiwa Kuwa, Na Jinsi Yasivyotakiw a Kuomba.**

*Dibaji*:

1. Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha. Mmoja katika wanafunzi wake walimwambia Bwana nini? Lk. 11:1; Mt. 6:9-13.
    a. Mitume wa Bwana walimwomba "Bwana utufundishe kuomba".
    b. Hili siyo ombi geni hata mmoja wetu angefanya hivyo, tungekuwapo, angelifanya vivyo hivyo. Jambo hili limetangazwa na kuelezwa mara kwa mara karne nyingi zilizopita, bado tunaona mwangwi wake unaendelea katika mioyo yetu.

2. Katika somo hili tutashughulikia kujifunza:
    a. Maombi (sala) yanavyotakiwa kutolewa.
    b. Maombi yasivyotakiwa kutolewa.

*Mazungumzo*:

I. Jinsi maombi yalivyo.
    a. Maombi ni haki ya upendeleo tuliyopewa pia ni amri tuliyopewa.
        1. Rom. 12:12
        2. Fil. 4:6
        3. Efe. 6:18
        4. 1 Thes. 5:17
        5. Ebr. 4:16.
    b. Maombi ni wakati wote na mahali pote kama mwanadamu alivyo, kama vile pale mwanzo nyakati za sethi, watu walipoanza kuliitia jina la Bwana, mwa. 4:26. Tusome katika Zab. 65:2.
    c. Kut. 22:23. Wakinililia nitawasikia, Kut. 22:27. Macho ya Bwana yanawaelekea wenye haki, Zab. 34:15.
    d. Maombi ni mashindano ya nafsi kushindania kumhitaji Mungu katika Zab. 42:1-2. Ni hali ya kawaida na ya asili ya mwanadamu kuwa na mahitaji ya kuomba au ya kutaka kuomba kama alivyo mtu mwenye njaa kutaka kula. Kushindwa kuomba kubaya zaidi ni kule kuto kutambua kuwa Mungu anajua yote.
    e. Sala ni upendeleo wa kumsihi Mungu, 2 Fal. 20:1-3; Mdo. 7:59, wa kuiweka roho kwa Mungu. Omb. 3:4; kuinua nafsi na kuipeleka juu; Zab. 25:1 na kuimwaga mbele zake, Zab. 62:8.
    f. "Maombi ni mbinu ya nafsi kujaribu kwa ukakamavu kuruka kwa mbawa zake kumtafuta Mungu kwa maarifa," J.J. Garrison.
    g. Maombi ni mahitaji ya kutoa kafara kwa Mungu aliye juu, kwa vitu vinavyokubalika kufuatana na mapenzi yake, kwa njia ya jina la Bwana Yesu.
    h. Wasomi wanatueleza kuwa, mwisho wa maombi huonyesha maneno mawili: nadhiri au kiapo, kimsingi au maneno ya awali, hili laonyesha kujiweka au kujitoa sisi wenyewe kwa Mungu kwa maombi au kwa nadhiri.

i. Alexander Cruden alisema kwamba “ombi au maombi” neno hili limetokana na neno la “interpellation” likiwa na maana ya mtetezi yaani mtu mwenye maombi ya kutetea.

II. Jinsi isivyotakiwa kuomba.

a. Maombi hayatakiwa kutolewa yasiyo na maana ya msingi kwa Mungu. Mara nyingi maombi yanatolewa kama mafarisayo waliofikiri kuwa watasikiwa kwa sababu ya sala zao kuwa ndefu, Mt. 5:7.
b. Maombi siyo ya dharura. Wengine hufanya maombi wanapokuwa na msiba au wakiwa na jambo lo lote la kutisha. Ifahamike kuwa maombi ni ya wakati wowote angalia Wafilpi 4:6.
c. Maombi hayamfanyi mtu awe mtii kipindi hicho, hasa mtu awapo mhitaji wa kazi mwenye kugeuza sikio lake lisisikilize sheria, ingawa sala yake ni ya machukizo angalia Mit. 28:9. Waona katika msalaba alipoangikwa Bwana, aliwaombea waliomwua, Lk. 23:34. Kwa sababu hawa watu hawakuwa na utii, Mdo. 2:22-41. Mungu atamsamehe kila dhambi ambayo anataka kuungama, 1 Yoh. 1:7-9. Ifahamike kuwa hatuwezi kumwomba Mungu amsamehe mtu ambaye hataki, 1 Yoh. 5:16.
d. Tusiwe na maombi ya kumweleza Mungu na wakati huo huo unamdharau mwanadamu. Akawatolea mfano akisema, Lk. 18:9-12. Waona mtu huyu alishuka kwenda nyumbani bila kusamehewa, Lk. 18:14.
e. Maombi siyo kuonyesha wengine mbele za Mungu huku tukificha mambo yetu mbele za Mungu, kwamba mambo yetu ni mazuri na yajibiwe.

**Swali na Jibu**

1. Je, Yesu aliwaambiaje wanafunzi wake walipomwomba awafundishe kuomba?

Asante: N. M. Lazima

## Hali Ya Maombi Yanayokubaliwa, No. 1

*Dibaji*:

1. Lk. 11:11 - Wanafunzi waliomba wafundishwe kuomba.

2. Maombi yaliyokubalika huifikia hali ya Mungu.

*Mazungumzo*:

I. Ni lazima yamwelekee Mungu, Baba yetu, Mt. 6:9.
- a. Sisi ni watoto wake, Rum. 8:14-15; 1 Yoh. 3:1-2.
- b. Wakristo wanaweza kuhakikishiwa ukweli mbali mbali kama tukiomba kwa Mungu.
  1. Anajua mahitaji yetu, Mt. 6:32.
  2. Anajua na anatoa zawadi, Mt. 7:11.
  3. Aliahidi kuwa Baba yetu.

II. Lazima yawe katika jina la Kristo.
- a. Kuna vifungu vingi vya kuthibitisha jambo hili, Yn. 16:13-14, 23-24; 1 Tim. 2:5; 1 Yoh. 2:1.
- b. Kila jambo tulifanyalo tulifanye katika jina Yesu, Kol. 3:17.

III. Ni lazima yatoke moyoni pamoja na roho ya msamaha.
- a. Yesu alifundisha hili, Mt. 6:12, 14-15; Lk. 17:3-4; Lk. 23:34; Mdo. 2:22-38; Efe. 4:31-32.

Asante: Heath Stapleton

**Hali Ya Maombi Yanayokubaliwa, #2**

*Dibaj*i:

1. Ni lazima kuelewa hali halisi ya maombi yanayokubaliwa.

*Mazungumzo*:

I. Maombi yawe katika hali ya kuyaelekea mapenzi ya Mungu-1 Yoh. 5:14-15.
- a. Omba kwa kufuata mapenzi ya Mungu naye atasikia.
- b. Umuhimu wa kufahamu na kuomba mapenzi ya Mungu - Mt. 7:21, 26:39, 42, 44; Yn. 4:34, 9:31.
- c. Nini maana kamili ya kuomba kufuatana na mapenzi ya Mungu?
  1. Kuambatanisha na kile alichotufundisha kuhusu sala. Kwa kuwa ni cha lazima na kina manufaa - Mt. 7:7-11.
  2. Yohana 11:42.

II. Sala (maombi) yawe katika imani.
- a. Mt. 21:22; Yak. 1:5-8.
- b. Kuomba kwa imani maana yake nini?
  1. Kwanza, inamaanisha Mungu ni Mungu - Ebr. 11:6.
  2. Pili, inaonyesha imani kwamba mungu humjali mtu Amwombaye - Mt. 10:29-30; Ebr. 4:14-16.
  3. Tatu, Mungu hujibu maombi yetu - Efe. 3:20; 2 Cor. 1:20.
  4. Kuomba kwa usahihi kunatuweka katika hali ya haki ili tupokee kile tunachokiomba.

Asante: Heath Stapleton

## Hali Ya Maombi Yanayokubaliwa, #3

*Dibaji*:

1. Dan. 6:4-9, 10.

*Mazungumzo*:

I. Maombi yafanyike kwa unyenyekevu - Lk. 18:9-14.
- a. Unyenyekevu maana yake-mtu kujishusha hali mwenyewe.
- b. Ombi la Farisayo lilikuwa katika hali ya ubinafsi - aya 9,11.
- c. Ombi la Farisayo lilikuwa katika tabia ya majivuno (kujikinai) - aya 12.
- d. Ombi la Farisayo lilikuwa ni moja ya kujikweza-aya 9,14.
- e. Ombi la mtoza ushuru lilikuwa la kujishusha na kunyenyekea - aya 13.
- f. Mtoza ushuru alijikabidhi na kumtegemea Mungu-aya 13.

II. Tuwe ndani ya Kristo kila tuombapo - Yn.15:7.
- a. Kuwa ndani ya kristo ina maana-kudumu/kuendelea/kukaa.
- b. Ulazima wa kuwa ndani ya Kristo - Yn. 15:4-5, 6, 7.
- c. Tunadumuje ndani ya Kristo - Yn. 15:10.

III. Tuombapo tutende haki - 1 Pet. 3:12.
- a. Mwenye haki ni nani? 1 Yoh. 3:7, 10; Zab. 119:172.

IV. Tuombapo tuzishike amri zake-1 Yoh. 3:22.
- a. Daima tuombe kuyajua mapenzi yake ili tumpendeze yeye, Yn. 4:34, 8:29; Efe. 5:17.
- b. Tukijua mapenzi yake, hatutamwomba jambo lo lote lililo kinyume.

V. Tuombe kwa bidii - Yn. 5:16.
- a. Eliya - Yak. 5:17.

Asante: Heath Stapleton

## Vizuizi Vya Maombi Yanayokubalika

*Utangulizi*:

1. Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa heshima, kama chombo kisicho na nguvu na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe, 1 Pet. 3:7.
    a. Somo letu linafunua kwamba maombi yetu yanaweza kuzuiliwa.
    b. Neno kuzuiliwa humaanisha kukatika au kukatishwa.

2. Maombi ni fulsa kubwa ya kila mtu kati yetu, lakini inasikitisha kiasi gani kuomba na maombi yasisikilizwe.

3. Baadhi ya mambo gani yanaweza kuzuia maombi yetu?

*Mjadala*:

I. Unafiki huzuia maombi yetu. Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amini nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha funga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi, Mt. 6:5, 6.
    a. Unafiki ni neno ambalo kimsingi huonyesha jibu; pia, kujifanya.
    b. Maombi ya mnafiki ni ya udanganiyifu. Anamdanganya mwanadamu mwenzake. Anaomba ili aonekane na watu wakati akijifanya mtakatifu; lakini anawadanganya. Anajidanganya yeye mwenyewe. Anapatata anacho kitafuta utukufu wa wanadamu-lakini hauna maana, kigeugeu na wa muda mfupi. Hapokei kitu toka kwa Mungu kama afikirivyo atapata.
    c. Maombi ya mnafiki ni ya ibada ya sanamu. Hawamwombi Mungu wa kweli, bali yeye mwenyewe amejiweka kuwa mungu wake na watu amewafanya sanamu, ambao anawataka wamtukuze. Katika kutafuta utukufu wa mwanadamu, anafanya kibali chao kishindane na ridhaa ya Mungu. Kosa kubwa katika maombi hayo, cha muhimu ni kwa ajili ya mimi mwenyewe badala ya yeye ninayemwomba.
    d. Baadhi ya zile sala au maombi mazuri ya siku hizi yanaangukia katika aina hiyo.
    e. Mtu afikiriapo sana namna aombavyo kuliko nini aombacho, ombi lake linakaukia juu ya midomo yake.

II. Kupayuka-payuka kunazuia maombi yetu. Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; Maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba, Mt. 6:7, 8.
    a. Kupayukua-payuka hutokana na neno ambalo humaanisha kugugumiza maneno, kusema kwa kubabaisha maneno na kisha kubwabwaja au kupiga

domo kwa kurudiarudia jambo lile lile mara nyingi.

1. Wafanya ibada ya Baali walimwita tangu asubuhi hata adhuhuri. 1 Fal. 18:26.
2. Watu wa muhamadia hurudia usemi wa tamko takatifu kwa masaa.

b. Kurudia kama kulivyo hakulaaniwi, kwa sababu Bwana wetu aliporudia maneno yale yale mara tatu katika Bustani ya Gethsemane, Mt. 26:44.

c. Kupayuka-payuka kunaonyesha uwingi wa maneno bila kufikiri wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi.

d. Maombi ya namna hiyo hujenga uzembe na kumchosha mfanya ibada na kudhani mungu hajali au hafahamu.

III. Dhambi huzuia maombi yetu.

a. Mwandika zaburi alisema; kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia, Zab. 66:18.

b. Isaya aliandika; tazama, mkono wa bwana haukupunguka, hata usiweze kuokoa; wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarakisha ninyi na mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msione, hata hataki kusikia. Isa. 59:1,2.

IV. Kuhifadhi kinyongo au kutosamehe kunazuia maombi yetu.

a. Ni lazima tuwasamehe wengine kama tungetaka kusamehewa. Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu, Mt. 6:14, 15.

b. Ni lazima tuwe macho daima kiasi gani tumesamehewa. Mfano wa Yesu katika Mathayo 18 ni dhahiri huonyesha kiasi gani Mungu ametusamehe sisi, na kiasi gani kidogo hatuko tayari kusamehe wakati mwingine. Matumizi ya mfano huo wa Yesu, yalikuwa, ndivyo na baba yangu wa mbinguni atakavyowatendea ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu na ndugu yake, Mt. 18:35.

c. Tabia ya kutosamehe itasababisha ibada ya mtu isikubaliwe na Mungu. Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu; Bali mimi nawaambia kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto. Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako, Mt. 5:21-24.

V. Ubinafsi huzuia maombi yetu. Vita vyatoka wapi, na mapigano yaliyoko kati yenu yatoka wapi? Si humu, katika tamaa zenu zifanyazo vita katika viuno vyenu? Mwatamani wala hamna kitu; mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata, mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi. Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu. Yak. 4:1-3.

a. Wakati mwingine hatupati tutakavyo kwa sababu twavitaka katika njia isiyostahili (mst. 2) au hatuombi kitu. (mst. 2 liganisha mt. 7:7).
b. Wakati mwingine maombi yetu ni ya kibinafsi.
    1. Mungu hatatoa kibali wakati ni ya kibinafsi, kwa ajili ya matashi ya kibinafsi. Kuomba isivyostahili kunavutwa na fikra duni, mbaya na za kibinafsi (Guy N Woods).
    2. Mungu anaona kilichotumika kwa ridhaa ya kibinafasi kama ufujaji na uharibifu.
    3. Ni rahisi (na yawezekana) mtu kuomba uwezo wa kuwatumikia wengine wakati nia kuu ya matashi hayo sio kwa kumfaidia mwanadamu, bali tamaa ya nguvu, umaarufu, utundu n.k. (Guy N. Woods).

VI. Mzozo wa familia huzuia maombi. Kadhalika ninyi waume kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe. 1 Pet. 3:7.
a. Kaeni limetafsiriwa kutoka usemi ambao unaonyesha ushirikiano wa nyumbani, na unajumlisha uhusiano wa hali ya ndoa.
b. Kwa akili humaanisha kuwa na ufahamu wa asili ya ushirikiano katika ndoa, kila mmoja akionyesha kumjali mwenzake, na kila mmoja akitenda kazi katika shughuli zao pekee.
c. Kumpa heshima maana yake ni kwamba waume ambao ni wakristo ni lazima wawaone wake zao ni wenye thamani sana na kuwapatia heshima istahirivyo.
e. Neno kuzuiliwa limefanyika kutokana na neno ambalo kwa kawaida humaanisha kukata au kukatisha. Mahali ambapo ugomvi na fitina vipo katika nyumba, maombi hukatika na kukatishwa ujumbe wa kwenda mbinguni umefanywa njia ya mkato! Uchungu, faraka na mabishano ni kinyume cha roho ya maombi na hufanya kazi ya kuzuia jitihada yote katika jambo hilo. Ni mahali pale tu penye amani na usawa vikitawala ndipo mume na mke wanapoweza kuunganisha nguvu za maombi kwenye Kiti cha Neema. (Guy N. Woods).

**Mjadala kwa njia ya maswali.**

1. Kwa nini ipo haja ya kujifunza mambo yale yanayoweza kuzuia maombi yetu?

2. Toa tafsiri ya unafiki kwa maneno yako mwenyewe?

3. Ni wapi aliposema yesu wanafiki hupenda kusali kwa nini?

4. Kwa nini yesu alisema wamepata thawabu yao?

5. Kwa nini maombi ya mnafiki ni ya udanganyifu kwa mwanadamu mwenzake?

Asante: Linkosi Mkwama

**Vitu Tunavyoweza Na Tungeweza Kuomba (Kusali) Kwa Ajili Yake, #1**

*Utangulizi*:

1. Biblia imejaa maagizo (maonyo) ya kuomba (kusali) bila kukoma, Efe. 6:18; Flp. 4:6; 1 Thes. 5:17.
   a. Yesu alifundisha haja ya kuomba siku zote, Lk. 18:1.

2. Paulo aliomba na ndugu zake (Mdo. 20:36-38), na akawaombea.
   a. Daima aliomba akiwa na kusudi maalum akilini.

*Somo Lenyewe*:

I. Tungeomba mapenzi ya Mungu yatimizwe.
   a. Yesu alifundisha hivi, mt. 6:10.
   b. Yesu aliomba hivyo, Mt. 26:42.
      1. Alisema "chakula" chake ni kufanya mapenzi ya Baba, Yn. 4:34.

II. Tungeomba kwa mahitaji ya maisha ya kila siku.
   a. Yesu alifundisha kwamba wanafunzi waombe kwa ajili ya mkate wa kila siku, Mt. 6:11.
   b. Ni mapenzi ya Mungu kwamba tuombe kwa ajili ya chakula chetu, lakini ni mapenzi yake pia kwamba tumwombapo tufanye kazi - Mwa. 3:19; 1 Thes. 4:11,12; 2 Thes. 3:10.
   c. Ni mapenzi ya Mungu kwamba tunaomba kwa ajili ya "mahitaji ya kila siku."
      1. Ni mapenzi ya Mungu pia kuwa tunaishi siku moja kwa wakati mmoja, Yak. 4:13-15.
      2. Hiyo inafanya maisha yawe na furaha na huru mbali na hofu, Mt. 6:24-34.

III. Tungeomba kwa ajili ya msamaha wa dhambi zetu.
   a. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kufanya hivyo, Mt. 6:12.
      1. Ni lazima ifahamike kwamba ni watoto wa Mungu tu ndio wenye haki ya kumwomba Mungu kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao.
         a. Wao, na wao tu, wana haki ya kusema "Baba yetu".
            1) Wengine wote na watoto wa Shetani, Yn. 8:44.
            2) Wengine wote wako katika ufalme wa giza, Kol. 1:13.
   b. Petro alimwamuru Simoni kuomba, Mdo. 8:22.
   c. Mungu anatuweka hali ya kuokolewa kwa njia ya kuenenda kwetu katika nuru kila siku na kukiri kila siku dhambi zetu, 1 Yoh. 1:7-10.

IV. Tungeomba kwa ajili ya msaada wa Mungu.
   a. Wakati wa kukumbwa na matatizo, 1 Sam. 8:1-7.
   b. Kwa kupata nguvu kupambana na kushinda majaribu, Mt. 6:13, 26:41;

1 Kor. 10:13; 2 Pet. 2:9.

c. Wakati wa huzuni na mawazo mazito (moyo mzito), Mt. 26:35-46.
d. Wakati wa kushughulika na kazi njema, Mdo. 13:1-3.
e. Wakati wa kuteseka, Yak. 5:13.
f. Tungeomba msaada wa Mungu wakati wote, Flp. 4:6.

V. Tungeomba kwa ajili ya wahubiri na kazi ya Bwana.

a. Paulo aliandika juu ya hilo, Rum. 15:30; Kol. 4:2, 3; 1 Thes. 5:25; 2 Thes. 3:1.
b. Si kila mtu anaweza kuhubiri, lakini kama haruni na huri walivyoishikilia mikono ya Musa wakati wayahudi wakiwa katika mapigano (Kut. 17:8-16), kila Mkristo anaweza kuiinua mikono ya mhubiri kwa njia ya sala (maombi).

Asante: Robert Stapleton

**Vitu Tunavyoweza Na Tungeweza Kuomba (Kusali) Kwa Ajili Yake, #2**

*Utanguliz* i:

1. Sala (maombi) ya kweli imeunganisha ndani yake kilio fulani cha msaada, Zab. 3, 6, 22, 30, 35, 41, 55-57, 64.
    a. Zab. 31.

*Somo Lenyewe*:

I. Tuombe kwa ajili ya watawala wa nchi.
    a. 1 Tim. 2:12; Rm. 13:1-3.

II. Tuombe kwa ajili ya ustawi wa mahali au mji tulipo (tunapoishi).
    a. Yer. 29:4-7; Zab. 122:6

III. Tuombe kwa ajili ya watenda kazi zaidi kuingia katika mavuno.
    a. Yn. 4:35-37; Mt. 9:37, 38.

IV. Tuombe kwamba wengine waweze kuokolewa.
    a. Rum. 10:1-3.

V. Tuombeane sisi kwa sisi.
    a. Rum. 1:9; 1 Kor. 1:4; Efe. 1:14, 16; Flp. 1:3, 4; Yak. 5:16.

Asante: Robert Stapleton

## Tabia Katika Sala (Maombi).

*Utangulizi:*

1. Nyakati zetu zimetajwa kuwa ni "kipindi cha jeti". Si kwa sababu tu ni cha utaratibu huu wa safari, bali pia kwa sababu tupo daima katika mwendo.

2. Ni kizazi cha mashaka na woga. Katika hali mbali mbali tumepoteza mwelekeo na fungamano letu na kujaribu kufunika mashaka yetu chini ya blanketi la sauti na mwendo.

3. Mtu wa kisasa anaonekana ana nyakati chache za utulivu na muda mfupi wa kutafakari. Lakini hata tuwe na mwendo wa kasi kiasi gani, au sauti ya kusikika kiasi gani, haviwezi kutufanya tusahau mahitaji yetu ambayo ni ya kweli kabisa. Tatizo letu sio jipya, wala jibu lake sio jipya.
   a. Isa. 30:15.
   b. Katika nchi yenye msukosuko, Mungu alitangaza katika Zab. 46:10.
   c. Kristo alizungumza na wanafunzi wake waliochoka alisema katika Mk. 6:31.
   d. Jibu la matatizo yetu mengi linaweza kupatikana katika utulivu wa sala (maombi) ambao unasisitiza umuhimu wa kujifunza yote ambayo tunaweza kuhusu jambo hili.

*Mjadala:*

I. Tabia yetu iweje katika sala (maombi)?
   a. Watu wa mashariki katika kipindi cha yesu walifanya makubwa kwa tabia katika maombi. Kulikuwa na sheria za kulitazama hekalu la sanamu zilizomwakilisha mungu. Kulikuwa na mazulia ya kusimama au kupiga magoti juu yake. Wakati mwingine mwombaji "aliinua juu mikono mitakatifu," wakati mwingine alikunja mikono. Mara nyingi sehemu yote ya waombaji iliweza kusujudu kwa kuinama chini kwa heshima kamili na unyeyekevu wote. Au kwa kuinama chini wakati viganja vya mikono viko juu ya zulia, kila ombi lifanyikapo mwombaji aligusa kichwa chake chini (sehemu ya paji la uso). Kila kitendo pekee kilikuwa na maana maalum na kutazamiwa kuleta baraka maalum (J.D. Murch, <u>Nifundishe Kuomba</u> Uk. 82).
   b. Ingekuwa ni vyepesi kuweka mkazo katika tabia ya kimwili kiasi kwamba inakuwa kama ni dawa fulani (kitu kama dawa) ambayo kwa kiasi kikubwa bila kujua tunaweka tumaini letu.
   c. Kulikuwa na nyakati ambazo watu walikaa na kuomba.
      1. I Fal. 19:4.
      2. I Nya. 17:16.
   d. Wakati mwingine watu waliomba wakiwa vitandani, 2 Fal. 20:1, 2.
   e. Yesu akaanguka kifulifuli, Mt. 26:39.

f. Paulo alipiga magoti, Mdo. 20:36.

g. Tusoma 1 Tim. 2:8, "Kuinua mikono iliyotakata" (mitakatifu) inahusu, kwanza tabia ambayo watu walikuwa nayo hapo awali wakati wa kuomba. Yasemekana kwamba walivielekeza viganja vyao mbinguni, katika hali ya kuomba (kuwania) msaada. Katika nafasi ya pili, maelezo yaonyesha haki kwa upande wa mwombaji. Hakuna mtu mwenye mikono yenye uchafu angejaribu kuongoza kusanyiko la wafanya ibada katika kusali kwa Mungu (Ayu. 17:9; Zab. 24:43; Yak. 4:8). Wale walioko katika sala ni lazima wawe mbali na uadui na uchungu baina yao, na mali na mzozo, yaani, mashaka na/au maswali kuhusu Mungu; ni lazima wawe na tumaini katika yeye (Ebr. 11:6) (Maoni ya somo la mwaka, apr. 13, 1958, uk. 82).

h. Kitendo (position) ambacho mtu anakionyesha (anakifanya) katika maombi sio lazima kiwe kipimio cha uhalali na ufanisi wa sala (maombi) yake, bali hali (ya nafsi) yake. "Kama kupiga magoti kutahamasisha moyo wa kweli wa mwombaji, basi natupige magoti. Kama kusimama na vichwa vimeinama huhamasisha moyo zaidi, basi miili yetu tuiweke hivyo. Wala kamwe tusijihisi katika dhamiri kwamba hali za tabia hizo ndizo zinazotupambanua na kutupatia kibali maalum katika maombi ama kwa mungu au kwa mwanadamu" (J.D. Murch).

II. Tabia gani ya kweli mtu awe nayo katika maombi.

a. Lazima kuwe na tabia ya kicho (heshima kuu).

1. Kamiusi ya Webster inatafsiri neno lialoelekeana na kicho: kuweka heshima ya juu pamoja na upendo....kuonyesha hali ya upendo na taadhima. Hutafsiri kuwa ni taadhima iliyoshuhudiwa; utoaji wa heshima uliotajwa bayana (wazi wazi) heshima nyingi iliyochanganyika na upendo....kujali au kutenda heshima ya ukuu zaidi.
2. Katika Agano la Kale, heshima hii hutokana na neno la **yare**, wazo la asili likiwa ni **kuogopa**. Hutumika kuelezea tabia mbele za Mungu mwenyewe na patakatifu pake (Zab. 89:7; Law. 19:30).
3. Neno hilo (kicho) pia latokana na neno **shadah** katika Agano la Kale, neno lake la msingi (chanzo chake) ni wazo la "kuanguka chini" kama kuinamisha mwili. Hutumika kuelezea mwinamo kujielekeza kwa mtu ambaye huchukuliwa kuwa ni wa heshima zaidi (2 Sam. 9:6; 1 Fal. 1:31; Est. 3:2).
4. Neno la agano jipya kuhusu neno hilo, hutoka katika neon **aidos** ambalo hujumuisha wazo la maadili na mwenendo mzuri (Ebr. 12:28; 1 Tim. 2:9; Tit. 2:3); **phobeomai** ambalo hujumuisha kuogopa au kujiweka chini ya mamlaka ipasavyo (Efe. 5); na **entrepomai** ambalo humaanisha wazo la "kujihesabu dhalili," na kuleta tabia ya kumheshimu mwingine (Mt. 21:37; Ebr. 12:9).

b. Lazima kuwe na tabia ya unyenyekevu.

1. Taratibu za talmud zinazo sehemu za maelezo kuhusu unyenyekevu ambao hufananishwa na tabia ya kufanya matoleo (sadaka) ambayo wafanya ibada walimtolea Mungu kabla hawajaanza ibada. Husema: "Yeye afanyaye matolea ya sadaka yote hupata thawabu ya sadaka yote; Yeye afanyaye matolea ya kuteketezwa atapata sadaka ya kuteketezwa; bali yeye afanyaye matoleo ya unyenyekevu kwa Mungu na mwanadamu atapata **thawabu** kama kwamba ametoa matoleo yote duniani."
2. Unyenyekevu wa mtoza ushuru (katika tabia yake ya unyenyekevu) kama alivyoomba mbele za Mungu ndio uliofanya sala ikubaliwe na Mungu (Lk. 18:13, 14).

c. Kuwe na tabia ya ukweli (uaminifu).

1. Ukweli (uaminifu) huo humaanisha pasipo hila, safi, halisi, nia safi, kweli. Nje ya udanganyifu, sio na unafiki (Webster).
2. Maombi ya wanafiki walioelezwa na Yesu katika Mat. 6:5-8, yalikataliwa kwa sababu nia yake haikuwa njema.

**Maswali ya mawazo na mjadala.**

1. Toa sababu angalau mbili kwa nini nyakati zetu huitwa "kipindi cha jeti"?

2. Kwa nini unafikiri kizazi chetu kinajipambanua mno kuwa katika mashaka na woga?

3. Tatizo letu kuu na ufumbuzi wake ni nini?

4. Ni tabia gani (baadhi) kuhusu maombi zilizoshikiliwa na baadhi ya watu wa mashariki wakati wa Yesu?

5. Ni juu ya jambo gani ingeonekana ni vyepesi kutilia mkazo zaidi?

6. Taja angalau tabia tano za kimwili ambazo watu wa biblia walizishikilia katika maombi?

7. Ni kitendo gani (physical position) huonekana kwako binafsi kama msaada unaokufanya uwe na tabia ifaayo unapofanya maombi (sala)?

8. Kusali (kuomba) na "mikono iliyotakata (mitakatifu)" maana yake nini?

Asante: B.J.M. Kulanga

**Baadhi Ya Matatizo Katika Maombi.**

*Utangulizi*:

1. Bila kufikiri nguvu ya maombi.
    a. Uchanga.
    b. Kutofuata taratibu za maombi.
    c. Kufikiri kuwa maombi ni kitu rahisi tu.
    d. Kufikiri kuwa unajua majibu ya maombi yote.
    e. Kutokuona matatizo yenyewe na unyoofu.

2. Suala hapa ni kupambana na matatizo katika maombi.
    a. Matatizo ya maombi.
        1) Hayazuki ghafula-hewani-wenyewe watu.
        2) Wengine wanadhani wanaweza:
            a. Kuyarahisisha
            b. Kuyakwepa
            c. Kujifanya hayapo
            d. Kukaa kimya.
        3) Matatizo yapo pale pale hayaondoki kwa mpango huo-mkato, Rum. 8:28. Wazo hapa ni kuwa:
            a. Vitu vyote vyema au mema tunafanya pamoja na Mungu.
            b. Kupinga yale maombi ambayo hayakubaliani na mpango halisi wa maandiko.

*Majadiliano*:

I. Baadhi ya vyanzo vya matatizo katika maombi.
    a. Ulegevu: kutotambua sheria ya mambo ya kiroho na kimwili.
    b. Mungu ameweka sheria kwa kila jambo-maombi.
    c. Kuishi maisha yanayofaa-kufuata sheria za Mungu alizoweka bila kuongeza au kuzipunguza.
    d. Ulimwengu-kiroho unaendeshwa vile vile na sheria.
    e. Ametoa sheria ya kumfanya mwenye dhambi awe Mkristo (Mk. 16:16).
    f. Ametoa sheria ya kumwabudu siku ya kwanza ya juma, ombi, meza, changizo, kujifunza na kuimba-haiwezi kubadilika.
        1. Mungu anayo sheria ya kiroho ya kutawala maombi.
            a. Kushindwa kuzielewa-matatizo ya wakristo kuvunjika mioyo.
            b. Maombi yao-kushindwa kujibiwa kama walivyotegemea.
            c. Tatizo lingine-kutokutii, kutokushika yale yanayofundishwa.
        2. Mwisho karibu sheria zote zinazotawala maombi yetu tutakayoendelea kuzizungumzia tumeisha ziongelea tayari.
    g. Maelezo na mafundisho ya wanadamu na hoja ni nyingi.
        1. Wengi wamekata tamaa na hawaombi.
        2. Lazima ujifunze biblia inaagiza nini juu ya maombi.

3. Biblia imeahidi nini katika maombi.

II. Je, Kuna uwezekano Mungu kujibu maombi yetu?

a. Wanadai Mungu habadiliki, ni kweli Mungu habadiliki, wanadondoa Yk. 1:17; Ebr. 13:8.

1. Maombi yawe dhaifu-Mungu hujibu tu.
2. Maombi bila utaratibu-Mungu hujibu tu.
3. Maombi ya kuiga na kurudiarudia-Mungu hujibu tu.

b. Wanadai kuwa kwa sasa miujiza ilikoma-ni kweli miujiza ilikoma, wanadondoa 1 Kor. 13:8-13; Efe. 4:7-16.

1. Mungu hawezi kujibu maombi-bila miujiza.
2. Mungu hawezi kujibu maombi-bila maajabu.
3. Wanaendelea kudai kuwa hiyo ni asili ya sheria yake.
   a. Wanasisitiza tu juu ya wazo la mtu.
4. Tuwe watii-katika kujifunza sheria za Mungu na bila kujali kiburi gani Mungu anafanya katika maombi yetu.

c. Hoja nyingine ni kuwa mungu anajua yote-hakuna ulazima kumwomba wanadondoa, Mat. 6:24-34.

1. Ni kweli Mungu anajua shida zetu zote-bado anatutaka tumwombe siku zote (1 Thess. 5:17-18), haya ni mapenzi yake soma Mt. 7:7-12; Yak. 4:1-3.
   a. Anajua mahitaji yote tunayohitaji.
   b. Anajua matatizo yatakayotupata.
   c. Anajua maisha yetu kuliko sisi wenyewe.
2. Wazazi wanajua watoto wao wanahitaji nini-kwa nini wawaombe?

d. Wanaendelea kudai, mungu anamjibu mtu akiomba namna yo yote na hali yo yote ile hakuna haja kuwa Mkristo.

1. Kama Mungu anamsikia na kumjibu kila mtu hakuna faida basi ya kuwa Mkristo-hoja hii ni mbovu na chafu.
2. Mungu hamsikii mwenye dhambi-nje ya kanisa-dhambi.

e. Wakristo nao hudai majirani wangu wa dini fulani: huomba sana tena kwa nguvu sana kwa sababu yule anapiga sana kelele katika maombi basi Mkristo uache kumwomba mungu sio kibali hicho.

1. Watu wengi wanapitia mlangoni hicho ni kibali cha sisi kuanza kupitia dirishani. Kama wao wanaomba ama vibaya au namna gani hicho sio kibali sisi kuacha kuomba.
2. Hiyo haizuii mkristo kuomba.

III. Nini baadhi ya matatizo katika maombi.

a. Kukosa imani-ni tatizo kuu, Yak. 1:6, maana yake nini?

1. Kusimama ndani ya neno la Mungu.
2. Ibrahimu na Sara (Rum. 4:19) wazee sana lakini walijua umuhimu wa:
   a. Ahadi za Mungu.
   b. Umuhimu wa imani.

c. Kumpa Mungu utukufu.
d. Walijua nini walichoahidiwa
3. Aliweza kufanikiwa soma, Rum. 4:20, 21.
4. Mungu anatutia moyo, Ebr. 4:14-16.
a. Tuombe kufuatana na mapenzi yake, 1 Yoh. 3:22, 5:14-15.
5. Katika matatizo haya wakulaumiwa sio Mungu bali sisi wenyewe.
6. Mara oh, mimi nina imani ndogo tu au sina imani kabisa. “Tunakwenda kwa imani si kwa kuona, 2 Kor. 5:7. Imani huja kwa kusikia neno la Kristo, Rum. 10:17.
7. Yak. 1:6.

b. Tatizo kubwa lingine ambalo mara kwa mara hujitokeza ni oh, mimi sijui Mungu anajibuje maombi.
1. Mifupa ya mtoto tumboni-unajua inavyokua? Hapana. Kutojua kwako (ujinga) kutazuia mifupa isikue tumboni?
2. Roho Mtakatifu anakaa ndani yako – Je, Unajua anavyokaa? Hapana. Ujinga huo wa kutokujua utamzuia Roho Mtakatifu asifanye kazi ndani yako?
a. Umeme na waya-huwezi kuona jinsi vinapounganika hiyo itazuia umeme usipite kwenye waya-gusa uone!
b. Radio yako Mbeya-mitambo Dar unajua na kuona jinsi radio yako inavyopokea-toka Dar? Hapana. Je, hiyo itazuia radio isiseme?
3. Wajibu wetu sisi ni kumwomba Mungu daima, anavyofanya mwachie yeye, Mhu. 11:5.
a. Je, Unaweza ukafahamu namna gani Mungu anajibu maombi pamoja na miujiza? Huwezi kufahamu....pamoja na miujiza, uliko namna gani mungu anajibu maombi bila miujiza au maajabu.

c. Tatizo la tatu na nne katika maombi ni: kurudia maneno uliyoomba tayari na kuomba omba msamaha (ibada sala zote lazima ziwe na utusamehe dhambi zetu).
1. Kama mmesema sala ya kwanza mungu tunaomba utusamehe inatosha, zaidi kilicho kibaya ni, “Tunaomba utsamehe makosa au dhambi zetu za tangu tulipozaliwa”.
a. Jamani! Ndugu, Mungu anasikia maombi yetu.
b. Ndugu! Mungu hasahau maombi tuliyokwisha mwomba iwe leo, jana juzi, wakati wo wote.
c. Mungu anasamehe dhambi zote za wakati wote.
1) Ubatizo-tunaposema hivyo tuna maana.
2) Kutubu-ubatizo hauondoi dhambi?
2. Tusiwashangae basi wale wanaoimba sala ya mfano ya Mat. 6.

IV. Kufuatisha maombi ya mtu mwingine (kuiga, mkumbo).

a. Kumbuka mahitaji yanatofautiana.

b. Kumbuka matatizo vile vile yanatofautiana.
c. Kumbuka mambo mengi yanatofautiana.
d. Mitume waliomba kutokana na hitaji lililowakabili kumbuka, Mdo. 1:24. Sio suala la kuigaiga tu, kumbuka mfalme Sulemani (1 Fal. 3:7, 9) aliomba kufuatana na hitaji la wakati ule.

Asante: J. D. Mwakyasima

**Je, Mungu Anajibu Maombi?**

*Dibaji*:

1. Inasemekana kuwa kati ya maombi mia sita sitini na saba katika Biblia, maombi mia sita hamsini na nne yana majibu kamili.

2. Watu wengine wameacha kuomba kwa sababu hawaamini kwamba Mungu anajibu maombi.

3. Watu wengine hawaombi kwa sababu hawaelewi ni jinsi gani Mungu anajibu maombi.

*Mazungumzo*:

I. Mungu ameahidi kujibu maombi.

a. Yesu alisema, "Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtaona; bisheni nanyi mtafunguliwa, " Mt. 7:7.

b. Tena yesu alisema, "Na lo lote mtakaloomba kwa jina langu, nitalifanya...." Yn. 14:13.

c. Mkiomba lolote kwa jina langu, nitafanya, Yn. 14:14.
d. Yohana aliandika, "Na lolote tuombalo twapokea kwake...." 1 Yoh. 3:22.
e. Na tukijua ya kuwa anatusikia, 1 Yoh. 5:14-15.
f. Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, amwombe Mungu awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei, naye atapewa, Yak. 1:5. hii inatukumbusha ahadi ya Bwana ya pekee katika Mt. 7:7, "Ombeni nanyi nitapewa." (Lk. 11:9). Hapa kuna ombi ambalo tunadhani Mungu atajibu, "na atapewa". Majibu katika maombi mengine yanategemea hali. Katika mifano fulani, ni lazima tutambue uwezekano kulingana na hali halisi ya ombi: "Kama inakupendeza, tunaomba ombi letu lipewe kibali." Kwa mfano, ilikuwa lazima kwamba Bwana wetu angerudi mbinguni. Kwa hiyo hapo bila kujali hata wanafunzi wake Yesu waliomba kwa moyo kuwa angebaki nao, lakini Yesu alirudi mbinguni. Ilikuwa imekusudiwa kuwa ni lazima aende zake (Yn. 16:7). Kwa kweli hakuna kitu kama hicho cha kusema Mungu hajibu maombi ya watu wake waaminifu. Anajibu kila ombi litolewalo na watoto wake. "Ni kweli," daima hasemi "ndiyo," mara nyingi husema "hapana". Lakini hiyo "hapana" ni jibu sawa na "ndiyo" na linatoka katika mfumo ule ule. Kwa mfano: mtoto kutokana na kupevuka (kukua) kwake anawaomba wazazi wake apate kibali ili akafanye mambo ya anasa kulingana na hali yake ya utoto aliyo nayo. Kukataa kwao juu ya hilo ombi la mtoto wao, si kwa nia ya kumkatisha tamaa mtoto asiombe vitu vingine, bali hilo ni jibu kwa

ajili ya ombi hilo tu, na jibu hutegemea ombi la mtoto hasa kuzingatia hali yake ya utoto. Katika hali hiyo hiyo, tunapofanya maombi yetu kwa Mungu ambayo matokeo yake siyo mazuri, au yanayolenga baraka za utajiri baadaye na Mungu hakutoa jibu la ombi hilo, hali hiyo haizuii maombi yetu mengine. Maana hilo ni jibu la ombi moja na jibu ni msaada kwetu sisi. Kwa hiyo tutambue hivyo na tuwe na hekima ya mungu tukifuata mifano hiyo. Guy N. Woods.

g. Mungu ameahidi kujibu maombi yetu na daima mungu hutimiza ahadi zake. 2 Kor. 1:20.

II. Kuna mifano mingi ambayo amejibu maombi.

a. Ibrahimu alimwomba Mungu amejibu maombi "Na Mungu aliwaponya Abimeleki na mkewe, pamoja na mjakazi wake, na wakazaa watoto, Mwa. 20:17.
b. Ayubu aliomba kwa ajili ya jamaa yake "Na Bwana akamrudishia miliki yake yote alipoomba kwa ajili ya jamaa yake. Pia Bwana akampa ayubu mara mbili ya alivyokuwa navyo kwanza, Ayu. 42:8-10.
c. Hezekia alikuwa mgonjwa karibu ya kufa, naye aliomba, "Nimesikia maombi yako, nimeyaona machozi hivyo nitakuponya....na nitakuongezea siku zako za kuishi, miaka 15."
d. Kuna mifano mingi ya Mungu kujibu maombi, hata kipindi cha miujiza, pasipo kuihusisha miujiza.
    1. Kwanza, Yakobo anasema, "Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, akaomba kwa bidii mvua isinye; na mvua haikunya juu ya nchi kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita," Yak. 5:17; 1 Fal. 17, 18. Je, hapo mungu alifanya muijiza? hapana! Sasa mvua ilikujaje? Kama ilinyesha pasipo mawingu basi huo ulikuwa ni miujiza. Kama ilitokea kwenye jangwa, basi huo ulikuwa miujiza, ilikujaje? Mawingu yalitokea baharini kama kila ifanyavyo kila mvua. Upepo ulivuma kuelekea mashariki, ulipokutana na baridi, mvuke wake ukawa katika hali ya maji, na mvua ikanyesha. Ilikuja kama mvua nyingine inavyokuja. J.W. McGarvey.
    2. Pili, Daudi alimwomba mungu alibadili baraza la Ahithofeli lionekane la kipumbavu. Hapo Daudi alifanya lile aliwezalo, Mungu alichukua nafasi na kulijibu ombi, lakini hapakuwa na ishara yo yote ya kimuujiza. Mungu alifanya hilo, lakini hatujui moja kwa moja kuwa alifanyaje, 2 Sam. 15:31, 32-34, 16:23, 17:7, 14.
    3. Tatu, Bwana aliwaambia wakristo kule yerusalemu alisema, "Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi wala siku ya sabato," Mt. 24:20. Mungu alijibu ombi hilo, lakini hakuna ushahidi kama muujiza ulifanyika.
e. Wakati mwingine mungu anajibu maombi yetu kwa kusema "ndiyo".
    1. Anaruhusu kuomba yale tuyaonayo kuwa ni mema kwetu na

yanaendana na mapenzi yake.

2. Wakati fulani anapokea maombi yetu si kwa sababu ni mazuri kwetu, bali kwa sababu tunakuwa na bidii ya kupata tumwombacho, 2 Sam. 8:1-9.
3. Wakati fulani Mungu husema "ndiyo" lakini asitupe sawa sawa na tulivyoomba.
    a. Yesu aliomba kikombe kimwepuke. Lakini Mungu hakukiondoa kikombe, ila alimpa nguvu za kukikamilisha , Lk. 22:42-43.
    b. Paulo alimwomba mungu amwondolee mwiba uliokuwa katika mwili wake. Mungu hakuondoa ule mwiba, ila alimpa nguvu za kuishi nao, 2 Kor. 12:7-9.
    c. Wakati mwingine tunaomba mawe, lakini Mungu hutupa mkate badala yake, Mt. 7:9-11.

f. Wakati fulani Mungu husema "hapana" katika maombi yetu, Yak. 4:1-4.
g. Wakati fulani anatutaka tusubiri kidogo. Paulo aliomba kwenda Rumi (Rum. 1:10), lakini jibu la ombi lake lilikuja miaka miiwili baadaye, Mdo. 27-28.
h. Siyo ombi kusema kuwa Bwana atafanya namna gani hili na lile, au kumdadisi Bwana ni jinsi gani atatubariki, hivyo tuelewe kuwa siyo swala letu kujua atafanyaje; ni ombi letu litakalomfanya yeye (Mungu) aamue anavyotaka. Tunayo imani: uhakika wa imani ambayo kwanza Bwana anaweza na anajibu maombi ya watakatifu, waombao kulingana na mapenzi yake, bila wao kutaka kuelewa Mungu atajibuje. Benjamin Franklin.
i. Mungu anajibu maombi yetu kufuatana na hekima yake isiyo na kipimo, siyo kulingana na mtazamo wetu ulio na kiwango maalum na uhaba wa kuelewa.

**Wazo na maswali ya mjadala.**

1. Kwa nini wengine wameacha kuomba?

2. "Omba utapewa" ni ombi linalolingana na hali au halilingani ?

3. Ni ahadi gani kuu ambayo Bwana aliiweka kwa wale waombao kwa jina lake?

4. Tunajuaje kuwa Mungu anajibu maombi yetu?

5. Ni nini ambacho wengi wetu tumepungukiwa na tunahitaji kumwomba Mungu atupatie?

6. Usemi huu una maana gani "Majibu ya maombi mengine hutegemea hali"?

7. Kwa nini Mungu hakuwajibu wanafunzi ombi lao la kumtaka Bwana akae nao duniani?

8. Hakuna kitu kama nini?

9. Ni katika njia ipi “hapana” katika maombi ni jibu sawa na “ndiyo” wakati fulani?

10. Mungu ameahidi kujibu maombi yetu. Kwa nini jambo hili linatupa faraja kubwa?

11. Kwa nini ibrahimu alimwombea Abimeleki?

12. Ayubu aliomba kwa ajili ya nani na kwa nini?

Asante: Peter Kamatula

## Vipi Kuhusu Maisha Yako Ya Maombi?

*Utangulizi* :

1. Yakobo 5:13-18, hutoa utajiri wa maelekezo kuhusu maombi.

*Somo Lenyewe*:

| I. Maswali ya kujipima | hapana | ndiyo |
| --- | --- | --- |
| a. Je, Maisha yangu ya maombi yanaridhisha? | ______ | ______ |
| b. Je, Uhusiano wangu kijamii unasaidia maisha yangu ya maombi? | ______ | ______ |
| c. Je, Uhusiano wangu katika shughuli unaafikiana na mapenzi ya Mungu? | ______ | ______ |
| d. Je, Anasa zangu zinakubaliana na ushirika na Mungu? | ______ | ______ |
| e. Je, Tabia yangu ya kusoma na kusikiliza kunaendeleza maisha ya maombi? | ______ | ______ |
| f. Je, Maisha ya nyumbani mwangu ni msaada au kizuizi katika ushirika na Mungu? | ______ | ______ |
| g. Je, Uhusiano wangu kidesturi unanisogeza zaidi kwa Mungu? | ______ | ______ |
| h. Je, Falsafa yangu ya maisha yanakubaliana na msimamo wa Ukristo katika maombi? | ______ | ______ |
| i. Je, Mwenendo wa imani na sala zangu za kidini zinakubaliana na mafundisho ya neno la Mungu? | ______ | ______ |
| j. Je, Ninatumia muda wa kutosha katika maombi? | ______ | ______ |
| k. Je, Ninaishi katika roho ya sala bila kulegalega kila saa na siku? | ______ | ______ |
| l. Je, Ninatumikishwa sana na vitu kiasi kwamba shughuli hizo za siku zinazuia maisha yangu ya sala? | ______ | ______ |
| m. Je, Ninadumisha tabia ya uchaji kwa Mungu wakati wote? | ______ | ______ |
| n. Je, Nimejitoa kwa moyo wote na juhudi katika maisha yangu ya maombi? | ______ | ______ |
| o. Je, Nayajua mafundisho yote ya Biblia kuhusu maombi? | ______ | ______ |
| p. Je, Najisikia kuhitimu katika taratibu za maombi kama zilivyofunuliwa ndani ya neno la Mungu? | ______ | ______ |
| q. Je, Kuna chuki yo yote ndani ya moyo wangu juu ya mtu ye yote? | ______ | ______ |

| | Hapana | Ndiyo |
|---|---|---|
| r. Je, Moyo wangu unaweka uchungu wa roho kwa Mungu au kwa mwanadamu mwenzangu? | ______ | ______ |
| s. Je, Namwendea Mungu katika maombi nikiwa na mashaka? | ______ | ______ |
| t. Je, Kuna dhambi yo yote maishani mwangu ambayo inaweza kuzuia uhusiano wangu na Mungu? | ______ | ______ |
| u. Je, Ninatoa wajibu wangu kikamilifu kama mtoto wa Mungu? | ______ | ______ |
| v. Je, Ninafahamu amani ya akili (mawazo) ambayo ni matunda ya uhusiano mzuri na Mungu? | ______ | ______ |
| w. Je, Ninaweza kusema dhahiri, "mapenzi yako yafanyike ndani yangu?" | ______ | ______ |
| x. Je, Nina fikra za uhusiano wa milele na Mungu? | ______ | ______ |

II. Nguvu ya maombi (sala).

a. Maombi ni jibu la Mungu kwa ajili ya hofu na wasiwasi, Flp. 4:6, 7.
b. Maombi yana nguvu ya kuhekimisha, Yak. 1:5, 6.
c. Maombi ni nguvu ya kufariji, 2 Kor. 1:3; Ebr. 5:7; Ebr. 4:14-16; 1 Pet. 5:7.
d. Maombi yana nguvu ya kusamehe, 1 Yoh. 1:7-10; Mdo. 8:22.
e. "Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana," Yak. 5:16b.

Asante: Robert Stapleton